# Kategoria ya Vimahali katika Lugha ya Kiswahili

**Fabiola Hassan**
Chuo Kikuu cha Dodoma
*fabiolahassan0@gmail.com*

***Ikisiri***
*Wanaisimu wa lugha ya Kiswahili wameainisha vimahali katika kategoria ya vielezi. Vimahali vinarejelea mahali tendo lilipotendeka, linapotendeka au litakapotendeka. Vilevile, ni vielezi kwa sababu vimeambikwa kiambishi tamati cha mahali –ni. Hata hivyo, matumizi ya vimahali katika tungo yanadhihirisha kuwa vina tabia za nomino. Makala haya yanabainisha kategoria ya vimahali katika Kiswahili kwa kuzingatia tabia zake za kisemantiki, kimofolojia na sintaksia kwa kuwa makala haya yanahusisha mofolojia, sintaksia na semantiki. Data za makala haya zimepatikana kwa mbinu ya uchambuzi wa matini mbalimbali za Kiswahili pamoja na upimaji wa usahihi wa kisarufi. Ufafanuzi wa data hizo umetumia nadharia ya Sampuli Kifani, ambayo inatoa fursa ya kuzichambua data zinazoonesha mwingiliano wa kikategoria pamoja na udarajia wa umemba katika kategoria za maneno. Makala yanabainisha kwamba kategoria ya vimahali hutegemea sifa za kisemantiki, kimofolojia na matumizi yake katika tungo. Hitimisho la makala haya ni kwamba vimahali ni maneno yenye mwingiliano wa kikategoria.*

**Maneno Muhimu**: Vimahali, vielezi, nomino, chagizo, kiima, yambwa, kijalizo

## 1.0 Utangulizi

Uaninishaji wa maneno katika kategoria mbalimbali ni utaratibu muhimu katika ufafanuzi wa lugha. Umuhimu huo unatokana na ukweli kwamba lugha imeundwa na maneno yanayotofautiana kikategoria. Maneno hayo ndiyo yanayotumika katika kuunda viambajengo vikubwa zaidi kama vile virai, vishazi na sentensi (O'Grady, 1997). Wanaisimu wanahitaji kategoria kwa ajili ya ufanunuzi wa kipengele fulani cha kiisimu kinachoshughulikiwa. Mathalani, tunapotaka kubainisha mofimu za neno lazima tujue kategoria ya neno hilo kwa sababu maneno ya kategoria tofauti hutofautiana kimofolojia. Kategoria za maneno ndiyo matofali ya kujengea ufafanuzi wowote wa kiisimu. Kutokana na umuhimu huo, tunapaswa kubainisha kwa usahihi kategoria za maneno mbalimbali ya lugha. Uainishaji wa maneno katika kategoria zake hufanywa kwa kutumia kigezo cha kisemantiki, kimofolojia na kisintaksia (Baker, 2003; Gleason, 1965; Taylor, 2003). Kwa hiyo, kigezo cha kisemantiki kinazingatia maana. Kigezo cha kimofolojia kinazingatia viambishi vya neno; na kile cha kisintaksia huzingatia mtawanyiko ama nafasi ya neno katika tungo pamoja na uamilifu.

Pamoja na umuhimu wake, uainishaji wa maneno una changamoto. Kuna wakati maneno huweza kuainishwa katika kategoria fulani, lakini kwa upande mwingine maneno hayo hayo yana sifa za kategoria nyingine. Vimahali, katika lugha ya Kiswahili,ni mfano wa maneno yenye tabia hiyo.Wanaisimu waliotangulia wa lugha ya Kiswahili wameainisha vimahali katika kategoria ya vielezi (Mdee, 1999) kwa kuwa vinarejelea mahali tendo lilipotendeka, linapotendeka au litakapotendeka. Pia, vimahali ni vielezi kwa sababu vinaambikwa kiambishi

tamati cha mahali *–ni*. Pamoja na uainishaji wao, matumizi ya vimahali katika tungo yanadhihirisha kuwa kuna wakati vimahali hutumika kama vielezi na wakati mwingine hutumika kama nomino. Makala haya yanabainisha kategoria ya vimahali katika lugha ya Kiswahili kwa kuzingatia tabia zake za kisemantiki, kimofolojia na kisintaksia.

## 1.1 Mbinu na Uchambuzi wa Data Kinadharia

Data zilizotumika katika makala haya zimekusanywa kwa mbinu ya upitiaji wa nyaraka zilizoandikwa kwa lugha ya Kiswahili pamoja na ile ya upimaji wa usahihi wa kisarufi wa tungo. Mtafiti alisoma matini mbalimbali zinazohusu sarufi ya Kiswahili ili kupata data zilizolengwa. Mifano ya matini ziliosomwa ni*Kitagulizi cha Mofolojia* (Wesana-Chomi, 2003), *Maendeleo ya Uhusika* (Khamis, 2008) na *Sarufi Maumbo ya Kiswahili* (Msanjila na wenzake, 2008). Mbinu hii ilimwezesha mtafiti kubaini kategoria ya vimahali kwa kuzingatia sifa zake. Katika mbinu ya upimaji wa usahihi wa kisarufi, mtafiti aliandaa tungo zenye vimahali vyenye dhima mbalimbali za kisarufi na kuviweka katika nafasi tofauti tofauti. Baada ya kuziandaa alifanya upimaji wa usahihi wa kisarufi wa tungo hizo kwa kutumia wanafunzi watano wa Shahada ya Umahiri ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Dar es salaam.

Mtafiti alitumia wanafunzi haokwa kuwa wanauelewa wa kutosha kuhusu sarufi ya lugha ya Kiswahili. Ufafanuzi wa data hizo umetumia misingi ya nadharia ya Sampuli Kifani ya Rosch (1977). Sampuli Kifani ni nadharia inayotumika katika kuchambua data zinazohusu ukategorishaji wa maneno ya lugha. Pia, Sampuli Kifani hufaa kuchambua data zinazoonesha mwingiliano wa kikategoria pamoja na udarajia wa umemba katika kategoria za maneno. Hivyo, imeweza kuonesha ni kwa

namna gani vimahali huweza kuwekwa katika kategoria mbalimbali za maneno kwa kuzingatia tabia zake za kisemantiki, kimofolojia na kisintaksia.

## 1.2 Dhana na Mtazamo Kuhusu Vimahali

Vimahali ni maneno au virai vinavyorejea mahali katika lugha. Miundo ya vimahali hutofautiana kati ya lugha moja na nyingine. Katika lugha nyingine zisizo za Kibantu kama vile Kilatini na Kicheki, vimahali huundwa na vihusika vya mahali *a* au *an*. Kwa mfano, Kilatini: *Esse Rom**a***‘to be at Rome’> *Ire Rom**an***‘to go to Rome’. Lugha nyingine kama vile Kiingereza hutumia vihusishi vya mahali. Kwa mfano, *He entered **in** the house*‘Alingia ndani ya nyumba’. Katika lugha za Kibantu kama vile Kichewa (N31), vimahali huundwa na viambishi vya ngeli za mahali 16 **pa*-, 17 **ku*-, 18 **mu*-, na 23 *i*[17]-. Viambishi hivi huambikwa mwanzoni mwa maneno hayo kama ilivyooneshwa katika mfano huu, ‘***ku***- *mudzi*’ ‘Kijijini’ (Bresnan & Kanerva, 1989). Katika lugha nyingine za Kibantu kama vile Kikuyu, vimahali huundwa kwa kiambishi tamati cha mahali kama vile *Nyungu-**ini*** ‘Ndani ya chungu’ (Rugemalira, 2004). Vilevile, katika lugha nyingine za Kibantu kama Kibena vimahali ambavyo ni majina mahususi ya mahali havina kiambishi cha ngeli ama kiambishi tamati cha mahali. Hivyo, miundo ya vimahali hutofautiana kati ya lugha moja na nyingine.

Kategoria ya vimahali ni suala lililozua mijadala miongoni mwa wanaisimu. Kuna wanaodai kwamba vimahali ni nomino kwa sababu kadhaa (Salzman, 2004). Mosi, vimahali vina uamilifu wa kiima, yambwa au kijalizo katika sentensi kama

[17] Kiambishi ngeli mahali ya 23 *i*- hujitokeza katika lugha chache na lugha hizo ni kama vile Kiganda.

ilivyo katika Mfano Na. 1(a) na 1(b). Pili, huukilia upatanishi wa kisarufi baina ya kimahali na vitegemezi vyake au baina ya kimahali na kitenzi kama ilivyo katika Mfano Na. 1(a) na 1(b):

1. a) *Chi-tsîmechi-li* ***ku-mu-dizi*** [Kichewa]
kng7-kisima kk7-kuwa kng17-kng3-kijiji
'Kisima kipo kijijini.'

b) ***Ku-mu-dizi*** ***ku****-li chi-tsîme*
kng17-kng3-kijiji Kk17-kuwa kng7-kisima
'Kijijini kuna kisima.'
**Chanzo:** Bresnan na Kanerva (1989:2).

Mfano wa 1(a) unaonesha kwamba kimahali *kumudzi* 'kijijini' kina uamilifu wa oblikyu mahali. Aidha, mfano wa1(b) unaonesha kwamba kimahali *kumudzi* 'kijijini' ni kiima.Kulingana na Rugemalira (2004) na Kahigi (2005), viambishi ngeli mahali ni vihusishi ama ni virai vihusishi kutokana na sababu mbalimbali. Mosi, viambishi hivyo huambikwa kwenye nomino ambayo ina kiambishi cha ngeli nyinginge kama ilivyo katika Mfano Na. 2. Pili, huweza kutengwa na shina la nomino kwa kutumia viyambo vingine katikati yake kama ilivyo katika Mfano Na. 3. Tukumbuke kwamba katika kirai maneno huwa pwekepweke na huruhusu uwekaji wa maneno katikati ya neno moja na lingine. Kwa kuwa kiambishi ngeli cha mahali huweza kutengwa na shina la nomino, basi kiambishi hicho ni kihusishi kinalojitegemea na, kwa, hivyo, kimahali kilichoambikwa kiambishi cha ngeli ya mahali ni kirai kihusishi. Tatu, viambishi vya kimahali havitumiki katika upatanishi wa kisarufi baina ya vitegemezi vyake kama ilivyo katika Mfano Na. 4(a). Badala yake, kiambishi cha ngeli ya nomino ambacho kilikuwapo kabla ya

uambikaji wa kiambishi cha ngeli ya mahali hutumika kama ilivyo katika Mfano Na. 4(b):

2. *a)* *a- **ba**ana* [Kinyambo]
kkk- kng2.toto
'Watoto'

*b)* *a-**mu**- **ba**ana*
kkk-kng18-kng2.toto
'Miongoni mwa watoto.'

3. *a)* *o-**mu**- **ba**ana*
kkk-kng18- kng2.toto
'Miongoni mwa watoto.'

*b)* *o-**mu**- baandi-**ba**ana*
kkk-kng18-kv2.engine-kng2.toto
'Miongoni mwa watoto wengine.'

4. *a) *o-**mu**- baana **mu**-bi*
kkk-kng18-kng2.toto kv2-baya
'Miongoni mwa watoto wabaya.'

*b)o-mu- **ba**ana **ba**-bi*

kkk-kng18-kng2.toto kv2-baya
'Miongoni mwa watoto wabaya.'
**Chanzo**: Rugemalira (2004).

Mfano wa 2(a) unaonesha nomino *abaana* 'watoto'. Nomino hii imeundwa na kiambishi cha ngeli ya pili kng2 *ba*-. Mfano wa2(b) unaonesha kwamba kiambishi cha mahali kng 18 *mu*- kimeambikwa katika nomino *abaana* 'watoto' ambayo ina kiambishi cha ngeli ya pili kng2 *ba*-. Kwa hiyo, vimahali huweza kuchukuliwa kama virai vihusishi kwa kuwa viambishi

vya ngeli za mahali huchukuliwa kuwa sio sehemu ya nomino bali ni kipashio kinachojitegemea ambacho huambikwa katika nomino iliyokamilika kimaumbo. Mfano wa 3(a) unaonesha nomino ya mahali *omubaana* ‘miongoni mwa watoto’ ambayo ina kiambishi cha ngeli ya mahali kng18 *mu*- pamoja na shina la nomino *baana* ‘watoto’. Mfano wa 3(b) unaonesha kwamba neno *baandi* ‘wengine’ limetokea katikati ya kiambishi cha ngeli ya mahali kng18 *mu*- na shina la nomino *baandi*.

Kiambishi cha ngeli ya mahali sio sehemu ya nomino *baana*na ndio maana kinaweza kutengwa na shina la nomino kwa kutumia kipashio kingine. Mfano wa 4(a) unaonesha kwamba kiambishi cha ngeli ya mahali kng18 *mu*- kikitumika katika upatanishi wa kisarufi na kivumishi *mubi* ‘wabaya’ kinazalisha tungo isiyokubalika. Kwa upande mwingine, mfano wa 4(b) unaonesha kwamba kiambishi cha ngeli nyingine kilichopo katika shina la nomino kng2 *ba*- kikitumika katika upatanishi wa kisarufi na kivumishi *babi* ‘wabaya’ kinazalisha tungo inayokubalika. Mifano hiyo inaonesha kwamba viambishi vya ngeli za mahali sio sehemu ya mashina ya nomino, bali ni vihusishi ambavyo vikiungana na mashina ya nomino huzalisha virai vihusishi. Wanaisimu wengine wameainisha vimahali kama vielezi (Mdee, 1999; Ngunga & Mpofu, 2013). Aidha, wanadai kwamba vimahali ni vielezi kwa sababu vinatoa taarifa ya tendo lilifanyika wapi kama inavyoonekana katika Mfano Na. 5. Kimofolojia, maneno hayo yameambikwa kiambishi cha ngeli ya mahali 16 *pa*-, 17 *ku*-, au 18 *mu*- ama kiambishi tamati cha mahali -*ni*. Mifano ya 5 na 6 inathibitisha hoja hii:

5. *Mw-anache* *ju-di* ***ku-cikoola***[Kiyao]
   Kng1-toto kk1-kuwa kng17-kng9.shule
   ‘Mtoto yupo shuleni.’

6. *Nyama ji-di **m'**-poto*
   Kng9.nyama kk9-kuwa kng19-chungu
   'Nyama imo ndani ya chungu.'

**Chanzo**: Ngunga na Mpofu (2013: 50).

Mfano wa 5 unaonesha kwamba kimahali *kuchikoola* 'shuleni' kinajibu swali la mtoto yuko wapi katika tungo hii. Aidha, mfano wa 6 unaonesha kwamba kimahali mpoto kimeambikwa kiambishi cha ngeli ya mahali kng18 *m-*. Kwa hiyo, washadidiaji wa mtazamo huu wanaeleza kwamba vimahali katika lugha ni vielezi. Licha ya kuwapo kwa mitazamo hii, kuna utata wa kategoria ya vimahali. Tatizo lililopo ni kwamba katika tungo za lugha moja, kuna wakati vimahali vinatumika kama vielezi na kuna wakati vinatumika kama nomino.

## 1.3 Nadharia ya Sampuli Kifani

Nadhari ya Sampuli Kifani iliasisiwa na mwanasaikolojia wa Kimarekani Eleanor Rosch katika miaka ya 1970 (Geeraerts, 1984). Msingi wa nadharia ya Sampuli Kifani ni memba ambaye ni mfano bora wa kategoria inayohusika. Katika kategoria kuna sampuli kifani mmoja au zaidi. Memba mpya anaingizwa katika kategoria iwapo anaonesha sifa zote au baadhi ya sifa za memba kifani wa kategoria hiyo. Pia, mwingiliano wa kategoria unatokana na kutokuwepo kwa mpaka baina ya kategoria moja na nyingine. Neno huweza kuonesha sifa za kategoria zaidi ya moja. Katika makala haya, msingi huu umetumika kuamua kategoria ya vimahali pale ambapo vimahali vinaonesha sifa za kielezi kwa upande mmoja na sifa za nomino kwa upande mwingine.

## 2.0 Vimahali katika Lugha ya Kiswahili

Sehemu hii inahusu vimahali katika lugha ya Kiswahili. Kwanza sehemu hii inaanza kubainisha miundo ya vimahali katika lugha ya Kiswahili, kisha inabainisha kategoria ya vimahali kwa kuzingatia sifa za kisemantiki, kimofolojia na kisintaksia.

## 2.1 Miundo ya Vimahali katika Lugha ya Kiswahili

Kwa kuzingatia data zilizokusanywa, vimahali katika Kiswahili vipo katika miundo mbalimbali. Kwanza, vimahali vingi ni maneno yaliyoambikwa kiambishi tamati cha mahali *-ni* mwishoni mwa mizizi yake. Polome (1967) anaeleza kwamba kiambishi tamati cha mahali *-ni* hufanya kazi badala ya viambishi vya ngeli za mahali.[18] Katika Mfano Na. 7, *pangoni* ni kimahali kilichoambikwa kiambishi tamati cha mahali *-ni*:

7. a) *Nyoka a-me-ingi-a**pango-ni**.*
   Kng1.nyoka kk1-kjn-ingi-kt kng5.pango-ktm
   'Nyoka ameingia pangoni.'

Hata hivyo, kuna Kigingi cha kisemantiki katika matumizi ya kiambishi tamati cha mahali *-ni*. Mathalani, kiambishi hiki hakiwezi kuambikwa katika nomino zinazorejelea wanyama ama kama inavyoonekana katika Mfano Na. 8. Hata hivyo, kuna nomino za wanyama au viumbe zinaweza kuambikwa kiambishi hicho. Nomino hizo ni zile zilizofanyiwa uleksishaji wa umahali na kuwa majina ya mahali kama ilivyo katika Mfano Na. (9):

8. *M-toto a-me-simam-a ***ng'ombe-ni**.*

[18]Lambert (1957) anaeleza kuwa viambishi vya ngeli za mahali hujitokeza katika nomino asili zinazorejelea mahali katika Kinjovu, Kingare, na lahaja za Mombasa *(pahali, kwahali*, na *mwahali)*.

Kng1.toto kk1-kjn-simam-kt kng1.ng'ombe-ktm
'Mtoto amesimama ng'ombeni.'

9. *M-toto a-me-end-a **Tembo-ni**.*
Kng1.toto kk1-kjn-end-kt kng1.tembo-ktm
'Mtoto ameenda Temboni.'

Mfano Na. 8 unaonesha kwamba uambikaji wa kiambishi *–ni* katika neno *ng'ombe* huzalisha neno lisilokubalika. Mfano Na. 9 unaonesha kwamba neno *Temboni* linakubalika katika Kiswahili.Pili, kuna vimahali ambavyo nivirai vilivyoundwa na vihusishi vya mahali. Vihusishi hivyo vinaweza kuwa sahili au changamani. Mifano ya vihusishi sahili ni *penye, kwenye, katika,* na *kwa* kama inavyoonekana katika Mfano Na. 10. Mifano ya vihusishi changamani ni *mbele ya, nyuma ya/kabla ya, juu ya, chini ya, kushoto, kulia, na pembeni*. Mfano wa 11 unaonesha virai vinavyorejelea mahali katika Kiswahili:

10. *Mi-ti mi-zuri i-po* ***penye nyumba***
Kng4-ti kv4-zuri kk4-kuwa penye kng9. nyumba
'Miti mizuri ipo penye nyumba.'

11. *Miti mi-zuri i-po* ***mbele ya nyumba***
Kng4-ti kv4-zuri kk4-kuwa mbele ya kng9. nyumba
'Miti mizuri ipo mbele ya nyumba.'

Katika mifano Na. 10 na 11, *penye nyumba* na *mbele ya nyumba* ni virai ambavyo ni vimahali. Tatu, kuna vimahali ambavyo ni majina mahususi yanayotaja miji, vijiji na nchi ambayo yanarejelea mahali katika lugha ya Kiswahili. Kwa kiasi kikubwa, majina hayo hayaambikwi kiambishi cha ngeli ya mahali, kiambishi tamati cha mahali -*ni*, au kihusishi cha mahali kama ilivyo katika Mfano Na 12. Hata hivyo, kuna

majina yanayotaja vijiji, kata na mitaa ambayo yameambikwa kiambishi tamati cha mahali *-ni* kama ilivyo katika Mfano Na. 13:

12. *Juma a-me-tok-a* ***Dodoma***
Kng1. Juma kk1-knj-tok-kt Dodoma
'Juma ametoka Dodoma.'

13. *Ashura a-me-end-a* ***Buguruni***
Kng1.Ashura kk1-knj-end-kt Buguruni
'Ashura ameenda Buguruni.'

Katika Mifano Na. 12 na 13, *Dodoma* na *Buguruni* ni mifano ya vimahali. Licha ya kuwapo kwa vimahali vyenye miundo hii yote, makala haya yameshughulikia kategoria ya vimahali ambavyo vimeundwa na kiambishi tamati cha mahali *-ni* pamoja na majina mahususi ya mahali.

## 3.0 Kategoria ya Vimahali kama Vielezi

Vimahali katika lugha ya Kiswahili ni vielezi. Vimahali ni vielezi pale vinapokidhi sifa za vilezi kisemantiki, kimofolojia, na kisintaksia kama ifuatazo:

### 3.1 Kisemantiki

Vimahali ni maneno yanayoeleza kuhusu mahali tendo lilipofanyika, linapofanyika ama litakapofanyika. Hueleza zaidi kuhusu tendo ambalo limekamilika katika taarifa zake za msingi. Kwa sababu hueleza tendo ambalo limekamilia, basi taarifa hiyo ni ya ziada tu na ikiondolewa haiathiri maana ya msingi ya sentensi. Mifano Na. 14(a) na (b) inathibitisha:

14. a) *M-toto a-na-li-a* ***ch-umba-ni***
Kng1-toto kk1-knj-mz-kt kng7-mz-ktm
'Mtoto analia chumbani.'
b) *M-toto a-na-li-a*
Kng1-toto kk1-knj-mz-kt
'Mtoto analia chumbani'.

Katika Mfano Na. 14(a), kimahali *chumbani*ni kielezi kwa sababu kinatoa taarifa kuhusu mahali tendo lilipotendeka. Mfano Na. 14(b) unaonesha kwamba uondoaji wa kimahali *chumbani* hakuathiri maana ya msingi ya sentensi. Hali hii ni kwa sababu kimahali hicho siyo sehemu ya muundo wa vishiriki vinavyokamilisha maana ya kitenzi *analia*. Kitenzi *analia* kinahitaji mliaji (mtenda) peke yake na katika muktadha wa sentensi hii mliaji ni *mtoto*. Katika muktadha huu kimahali *chumbani* sio sehemu ya kitenzi hicho.

## 3.2 Kimofolojia

Kama Mdee (1999) anavyoeleza kwamba vimahali ni vielezi kwa sababu ni maneno yanayoambikwa kiambishi tamati cha mahali -*ni*. Mfano Na. (15) unathibitisha:

15. *M-toto a-na-som-a* ***ch-umba-ni***
Kng1-toto kk1-knj-mz-kt kng7-mz-ktm
'Mtoto anasoma chumbani.'

Katika Mfano Na. 15, kimahali *chumbani* kimeishia na kiambishi tamati cha mahali -*ni*. Hivyo, kimofolojia kimahali *chumbani*ni kielezi. Maneno mengine ni kama vile *darasani*, *mezani*, *ukumbini* na *ubaoni*. Hata hivyo, kigezo cha kimofolojia kinaweza kusailika. Hali hii ni kwa sababu katika lugha ya Kiswahili, kuna aina kadhaa za vimahali kama

tulivyoona katika sehemu iliyotangulia. Je, vimahali ambavyo ni majina mahususi ya mahali ambayo hayaishii na kiambishi tamati cha mahali *-ni* haviwezi kuwa vielezi? Data inatuonesha kwamba kwa kutumia kigezo cha kisemantiki ama sintaksia, vimahali hivyo pia huweza kuwa vielezi.

### 3.3 Kisintaksia

Kisintaksia, vimahali ni vielezi kwa kuzingatia sifa kadhaa. Mosi, vinaweza kuwa na dhima ya chagizo katika tungo. Chagizo ni dhima ya kisarufi ambayo inafanywa na kiambajengo ambacho kinaeleza kuhusu kitenzi ambacho kimekamilika kimuundo wake. Taarifa hiyo huwa ni maelezo ya ziada kuhusu kitenzi hicho kwa sababu haikamilishi semantiki ya kitenzi na sio sehemu ya muundo wa vishiriki vya kitenzi. Aidha, kwa kuwa ni taarifa ya ziada, basi huweza kuwapo au kuondolewa bila kuleta athari ya maana ya msingi katika tungo inayohusika. Mfano Na. 16 unathibitisha hoja hii:

16. *Jumaa-na-chek-a* ***ofisi-ni***
    Kng1.Juma kk1-knj-mz-kt kng9.ofisi-ktm
    'Juma anacheka ofisini.'

Katika Mfano Na. 16, kimahali *ofisini*ni chagizo. Hii ni kwa sababu kimahali hicho siyo sehemu ya muundo wa vishiriki vinavyokamilisha maana ya kitenzi kinachounda sentensi hii *cheka*. Kitenzi *cheka* kinahitaji mchekaji (mtenda) peke yake, na katika muktadha wa sentensi hii mchekaji ni *Juma*. Kwa upande mwingine, kitenzi hicho wala hakihitaji kujalizwa na taarifa ya mahali tendo linapofanyika. Katika muktadha huu kimahali *ofisini* sio cha lazima. Pili, kisintaksia, kimahali ni kielezi iwapo kinaweza kuhamishika kutoka sehemu moja ya sentensi kwenda sehemu nyingine bila kuathiri wala kubadili

dhima za kisarufi za viambajengo vya sentensi inayohusika. Mfano Na. 17 unathibitisha hoja hii:

17. ***Ofisi-ni**, Juma a-na-chek-a*
kng9.ofisi-ktm kng1.Juma kk1-knj-mz-kt

'Ofisini, Juma anacheka.'

Katika Mfano Na. 16, tunaona kwamba kimahali *ofisini* kimetokea baada ya kitenzi *anacheka*; lakini, katika Mfano Na. 17 tunaona kuwa kimahali hicho kimehamishwa na kutokea kabla ya mtenda *Juma*. Licha ya kutokea katika nafasi hii, kimahali hicho kina dhima ile ile ya kisarufi ambayo ni chagizo. Pia, mtenda *Juma* ana dhima ile ile ya kisarufi ambayo ni kiima. Aidha, Hivyo, kimahali ni kielezi iwapo ni chagizo. Pia, kimahali hicho kiwe na uwezo wa kuhamishika kutoka sehemu moja kwenda nyingine bila kuathiri dhima yake ya kisarufi au dhima za kisarufi za viambajengo vingine katika tungo.

## 4.0 Kategoria ya Vimahali kama Nomino

Licha ya kwamba vimahali ni vielezi, pia ni nonimo kwa kuzingatia sifa za kisemantiki, mofolojia na sintaksia kama ifuatavyo:

### 4.1 Kisemantiki

Kisemantiki, vimahali ni nomino kwa sababu hutaja majina ya mahali. Mahali hapo panaweza kuwa pa jumla, mahususi ama ndani kama inavyoonekana katika Mfano Na. 18:

18. a) ***Ofisi-ni**pa-na-pendez-a*
kng9.ofisi-ktm kng16-knj-pendez-kt

'Ofisini panapendeza.'

b)***Ofisi-ni*** *ku-na-pendez-a*
kng9.ofisi-ktm kng17-knj-pendez-kt
'Ofisini kunapendeza.'

Mfano Na. 18(a) – 18(b) inaonesha kwamba neno 'ofisini' katika mifano yote mitatu linataja mahali pa jumla, mahususi na ndani mtawalia. Hivyo, kisemantiki, vimahali ni nomino.

## 4.2 Kimofolojia

Kimofolojia, vimahali ni nomino kwa kuwa vimeambikwa kiambishishi tamati cha mahali -*ni* ama kiambishi kapa (iwapo ni majina mahususi ya mahali). Maneno haya yanatokea katika ngeli ya 16, 17 na 18. Yanatoka katika ngeli hizo kwa kuwa yanatumia vipatanishi vya ngeli ya 16 *pa*-, 17 *ku*-, na 18 *mu*-. Mifano Na. 18 na 19 inathibitisha hoja hii:

19. a) ***Dodoma pa****-na-pendez-a*
Kng16. Dodoma kng16-knj-pendez-kt

'Dododma panapendeza.'

b) ***Dodomaku****-na-pendez-a*
Kng17.Dodoma kng17-knj-pendez-kt

'Dodoma kunapendeza.'

Mifano Na. 18 unaonesha kwamba *ofisini* ni kimahali kilichoambikwa kiambishi tamati cha mahali *–ni*, lakini Mfano Na. 19 unaonesha kuwa *Dodoma* ni kimahali chenye kiambishi kapa cha mahali. Aidha, vimahali *ofisini*na*Dodoma* vinaukilia upatanishi wa kisarufi kwa kutumia kiambishi cha ngeli ya 16 *pa*-, 17 *ku*-, na 18 *mu*-. Kimofolojia, vimahali ni nomino zinazotokea katika ngeli ya 16, 17 na 18.

## 4.3 Kisintaksia

Kisintaksia, kimahali hudhihirisha dhima za kisarufi zinazofanywa na nomino. Dhima ya kwanza ni kwamba kimahali huweza kuwakiima. Kimahali kinapokuwa kiima kinadhihirisha tabia za kiima kama zilivyoelezwa na Keenan (1976a), TUKI (1990), Van Valin (2001), Kroeger (2005) na Mkude (2005). Sifa ya kwanza ni kwamba katika mfuatano wa kawaida wa viambajengo katika sentensi, kimahali hutokea mwanzoni kabla ya kitenzi. Pili, kimahali huweza kuukilia upatanishi wa kisarufi na kitenzi kwa kutumia kiambishi cha ngeli ya mahali. Mfano Na. 20 unathibitisha hoja hizi mbili:

20. ***Ki-wanja-nipa***-*me-ot-a nyasi*
kng7-wanja-ktmkk16-ktmlf-ot-ktkng9.nyasi
'Kiwanjani pameota nyasi.'

Mfano Na. 20 unaonesha kuwa kimahali *kidevuni* kimetokea mwanzoni mwa sentensi kabla ya kitenzi *pameota*. Pia, kimahali hicho kinaukilia upatanishi wa kisarufi na kitenzi kwa kutumia kiambishi cha upatanishi wa kiima cha ngeli ya 16 *pa*-. Aidha, kiambishi cha upatanishi wa kimahali na kitenzi hubadilika kulingana na mabadiliko ya dhana ya kimahali ama ngeli ya kimahali kilichotumika. Mifano Na. 21(a), (b), na (c) inathibitisha hoja hii:

21. a) ***Ukumbi-ni pa***-*me-pamb-w-a ma-ua*
kng14.ukumbi-ktmkk16-ktmlf-pamb-ktndw-kt
kng6-ua
'Ukumbini pamepambwa maua.'

b) ***Ukumbi-niku***-*me-pamb-w-a ma-ua*
kng14.ukumbi-ktmkk17-ktmlf-pamb-ktndw-kt
kng6-ua
'Ukumbini kumepambwa maua.'

c) ***Ukumbi-nim***-*me-pamb-w-a ma-ua*
kng14.ukumbi-ktmkk18-ktmlf-pamb-ktndw-ktkng6-ua
'Ukumbini mmepambwa maua.'

Mfano wa 21(a) unaonesha kwamba kiambishi cha ngeli ya 16 *pa*- kimetumika kama kiambishi cha upatanishi baina ya kimahali *ukumbini* na kitenzi *pamepambwa*. Mfano wa21(b) unaonesha kwamba kiambishi cha ngeli ya 17 *ku*- kimetumika kama kiambishi cha upatanishi wa kisarufi baina ya kimahali *ukumbini* na kitenzi *kumepambwa*. Mfano wa21(c) unaonesha kwamba kiambishi cha ngeli ya 18 *mu*- kimetumika kama kiambishi cha upatanishi baina ya kimahali *ukumbini* na kitenzi *mmepambwa*.Sifa ya tatu ni kwamba kimahali ambacho ni kiima cha kishazi bebwa huweza kurejeshwa na kuwakilishwa na kiambishi cha urejeshi katika kitenzi. Kimahali hicho huweza kurejeshwa iwapo kinafanana na kiima cha kishazi kikuu kama ilivyo katika Mfano Na. 22:

22. Kijijini [Kijijini kumeenea ugonjwa] kumejaa watu
Kijijini [kulikoenea ugonjwa] kumejaa wageni

*Ki-jiji-ni ku-li-**ko**-ene-a u-gonjwa ku-me-ja-a wa-geni*
kng7-jiji-ktm kk17-knj-krj17-ene-kt kng14-gonjwa kk17-ktmlf-ja-kt kng2-geni
'Kijijini kulikoenea ugonjwa kumejaa wageni.'

Mfano Na. 22 unaonesha kuwa kimahali *kijijini* ni kiima cha sentensi bebwa *Kijijini kumeenea ugojwa*. Nomino hiyo inarejeshwa na kuwakilishwa na kirejeshi *–ko*- katika kitenzi *kulikoenea*. Sifa nyingine ni kwamba kimahali kinapokuwa

kiima cha kishazi kikuu huweza kuhusishwa na kiima cha kishazi jalizi. Mfano Na. 23 unathibitisha hoja hii:

23.*Bahari-ni ku-na-on-ek-an-a ku- me-ja-a maji*
kng9.bahari-ktm kk17-knj-on-ktndk-ktndn-kt kk17-ktmlf-ja-kt kng5- maji
'Baharini kunaonekana kumejaa maji.

Mfano Na. 23 unaonesha sentensi ambayo imeundwa na kishazi kikuu *baharini kunaonekana* pamoja kishazi jalizi *kumejaa maji*. Kiima cha kishazi kikuu ni kimahali *baharini* na kiima cha kishazi jalizi hakiko wazi. Hata hivyo, sifa za kiima cha kishazi kikuu zinafanana na sifa za kiima cha kishazi jalizi. Hali hii ni kwa sababu katika kishazi kikuu, kiima *baharini* kinaukilia upatanishi wa kisarufi na kitenzi kinaonekana kwa kutumia kiambishi cha upatanishi wa kiima cha ngeli ya 17 *ku-*. Kwa upande mwingine, katika kishazi jalizi, kiima kisicho dhahirikinaukilia upatanishi wa kisarufi na kitenzi *kumejaa* kwa kutumia kiambishi cha upatanishi wa kiima cha ngeli ya 17 *ku-*. Hivyo, sifa za kiima cha kishazi kikuu zinafanana na sifa za kiima cha kishazi bebwa.Dhima ya pili ni kwamba kimahali huweza kuwa yambwa kama inavyoonekana katika Mfano Na. 24. Kimahali kinapokuwa yambwa kinadhihirisha tabia za yambwa katika lugha kibantu kama zilivyoelezwa na Hyaman na Duranti (1982):

24. *Mama a-na- pend-a* ***m-jini***
Kng1.mamakk1-knj-pend-kt kng3-jini
'Mama anapenda mjini.'

Mfano Na. 24 unaonesha kuwa kimahali *mjini* kina dhima ya kisarufi ya yambwa. Kimahali kinapokuwa yambwa

kinadhihirisha tabia za yambwa. Mosi, huweza kuwekewa kiambishi yambwa kama ilivyo katika Mfano Na. 25. Hata hivyo, kiambishi yambwa huambikwa kwenye kitenzi kwa kuzingatia vigezo vitatu. Kwanza, iwapo nomino yenye dhima ya yambwa hutoka katika ngeli ya kwanza au ya pili. Pili, iwapo nomino hiyo ina sifa ya uhisivu; yaani, inarejelea kirejelewa ambacho ni binadamu au mnyama. Tatu, iwapo nomino hiyo ina umahususi. Kwa upande mwingine, kiambishi yambwa huwa ni cha hiari iwapo nomino yenye dhima ya yambwa haijakidhi vigezo hivi. Kwa mfano:

25. *Mama* *a-na-* ***pa****-pend-a* ***m-jini***
Kng1.mama kk1-knj-ky16-pend-kt kng3-jini
'Mama anapapenda mjini.'

Mfano Na. 25 unaonesha kuwa kimahali *mjini* kimewekewa kiambishi yambwa *–pa-* katika kitenzi *anapapenda*. Hata hivyo, kiambishi hicho huwa ni cha lazima iwapo kimahali *mjini* ni mahususi na mzungumzaji anajua kwamba anarejelea *mjini* gani. Hivyo, vimahali ni nomino kama zilivyo nomino nyingine katika lugha ya Kiswahili. Pili, kimahali kinapokuwa yambwa huweza kuwa kiima cha sentensi tendwa. Mfano Na. 26 unathibitisha hoja hii:

26. a) *Mamaa-na-pend-a* ***m-jini***
Kng1.mamakk1-knj-pend-ktkng3-jini
'Mama anapapenda mjini.'

b) ***M-jini****pa-na- pend-w-a na Mama*
Kng3-jini kk16-knj-pend-ktndw-ktnakng1. mama
'Mama anapapenda mjini.'

Mfano Na. 26(b) unaonesha kuwa kimahali *mjini*ni kiima cha sentensi tendwa na kimetokea kabla ya kitenzi *panapendwa*. Hivyo, vimahali huweza kuwa nomino kama zilivyo nomino nyingine katika Kiswahili. Tatu, kimahali kinapokuwa yambwa huweza kurejeshwa na kuwakilishwa na kiambishi cha urejeshi kinachoambikwa katika kitenzi. Mfano Na. 27(b) unathibitisha hoja hii:

27. a) *Mamaa-na- pend-a* ***m-jini***
Kng1.mamakk1-knj-pend-ktkng3-jini
'Mama anapapenda mjini.'

b) *Mamaa-na- pend-a* ***m-jini*** *pa-li-**po**-pand-w-a ma-ua*
Kng1.mama kk1-knj-pend-ktkng3-jini kk16-knj-krj16-ktndw-kt kng6-ua
'Mama anapenda mjini palipopandwa maua.'

Mfano Na. 27(b) unaonesha kuwa kimahali *mjini* ambachao ni yambwa katika tungo kimeweza kurejeshwa na kuwakilishwa na kiambishi rejeshi -*po*- ambacho kimeambikwa katika kitenzi *palipopandwa*. Hivyo, ni dhahiri kwamba vimahali huweza kuwa nomino kama zilivyo nomino nyingine katika lugha ya Kiswahili. Dhima ya tatu ni kwamba kimahali huweza kuwa kijalizo cha kirai kihusishi. Kirai kihusishi ni kirai ambacho kimeundwa na kihusishi kama neno kuu pamoja na kijalizo. Kimahali nacho huweza kutumika kama nomino kwa kuwa kijalizo cha kirai kihusishi kama inavyoonekana katika Mfano Na. 28:

28. *Juma a-me-m-pig-a m-toto wa**m-ji-ni***
Kng1.Juma kk1-ktmlf-ky1-pig-kt kng1-toto wa kng3-ji-ktm

'Juma amempiga mtoto wa mjini.'

Katika Mfano Na. 28 tunaona kuwa kiambajengo *wa mjini* ni kirai kihusishi ambacho kimeundwa na kihusishi *na* pamoja na kijalizo ambacho ni kimahali *mjini*. Kwa hiyo, kijalizo cha kirai kihusishi hiki ni kimahali. Vilevile, licha ya kudhihirisha dhima za kisarufi za zinazofanywa na nomino, kimahali huukilia upatanishi wa kisarufi na vitegemezi vyake. Kimahali, kinapotumika kama kiima, yambwa, au kijalizo huukilia upatanishi wa kisarufi na vitegemezi vyake. Kitegemezi cha kwanza ni kioneshi kama ilivyo katika Mfano Na. 29:

29. *Ki-jiji-ni kule ku-me-ene-a u-gonjwa*
Kng7-jiji-ktm kko17.kule kk17-knj-ene-kt kng14-gonjwa
'Kijijini kule kumeenea ugonjwa.'

Mfano Na. 29 unaonesha kwamba kimahali *kijijini* ambayo ni kiima kinaukilia upatanishi wa kisarufi na kioneshi *kule* kwa kutumia kiambishi cha upatanishi wa kioneshi cha ngeli ya 17 *ku*-. Ikumbukwe kwamba tabia ya kimahali kuukilia upatanishi wa kisarufi na kioneshi hujitokeza pia iwapo kimahali kinatumika kama yambwa au kijalizo. Kitegemezi cha pili ni kimilikishi. Kimahali, kama ilivyo nomino, huukilia upatanishi wa kisarufi na kimilikishi kama ilivyo katika Mfano Na. 30:

30.*Ki-jiji-ni kw-angu ku-me-ene-a u-gonjwa*
Kng7-jiji-ktm kkm17.kule kk17-knj-ene-kt kng14-gonjwa
'Kijijini kwangu kumeenea ugonjwa.'

Mfano Na. 30 unaonesha kwamba kimahali *kijijini* ambacho ni kiima kinaukilia upatanishi wa kisarufi na kimilikishi *kwangu* kwa kutumia kiambishi cha upatanishi wa kimilikishi cha ngeli

ya 17 *kw*-. Ikumbukwe kwamba tabia ya kimahali kuukilia upatanishi wa kisarufi na kimilikishi hujitokeza pia, iwapo kimahali kinatumika kama yambwa au kijalizo. Kitegemezi cha tatu ni kihusianishi. Kimahali, kama ilivyo nomino, huukilia upatanishi wa kisarufi na kivumishi kama inavyoonekana katika Mfano Na. 31.

31.*Asha a-me-ka-a sakafu-ni pa-chafu*
Kng1.Asha kk1-ktmlf-ka-kt kng9.sakafu-ktm kv16-chafu
'Asha amekaa sakafuni pachafu.'

Mfano Na. 31 unaonesha kuwa kimahali *sakafuni* kinaukilia upatanishi wa kisarufi na kivumishi *pachafu* kwa kutumia kipatanishi wa kivumishi cha ngeli ya 16 *pa*-. Kuhusu suala la upatanishi wa kisarufi, imebainika kwamba nomino huukilia upatanishi wa kisarufi na kishazi rejeshi kinachofanya kazi ya kivumishi katika sentensi. Hoja hii inathibitishwa na Mfano Na. 32:

32. *Sakafu-ni* ***pa-li-po-tandik-w-a zuria*** *pa-me-chafuk-a*
kng.sakafu-ktm kk16-knj-krj16-tandk-ktndw-kt kng5.ziria kk16-ktmlf-chafuk-kt
'Sakafuni palipotandikwa zuria pamezagaa taka.'

Mfano Na. 32 unaonesha kuwa kimahali *sakafuni* kinaukilia upatanishi wa kisarufi na kishazi rejeshi *palipotandikwa zuria* ambacho kinafanya kazi kama kivumishi kwa kutumia kiambishi cha upatanishi wa kiima cha ngeli ya 16 *pa*-. Hata hivyo, ikumbukwe kwamba kimahali kinapotumika kama kiima, hakiukilii upatanishi wa kirarufi na kishazi rejeshi kinachofanya kazi kama kivumishi tu, bali pia kinaukilia upatanishi wa kisarufi na kitenzi kwa kutumia kiambishi cha

upatanishi kile kile kilichotumia katika kishazi rejeshi. Hivyo, kwa kuzingatia data, vimahali katika Kiswahili ni nomino kwa sababu vinadhihirisha tabia za nomino nyingine kisemantiki, kimofolojia, na kisintaksia.

## 5.0 Hitimishona Mapendekezo

Data za makala haya zimeonesha kwambakatika lugha ya Kiswahili vimahali huweza kuwa katika miundo mbalimbali kwa kuzingatia namna vimahali vinavyoambikwa kiambishi tamati cha mahali *-ni*, vinavyoundwa na vihusishi vya mahali ama majina mahususi ya mahali. Kuhusu kategoria ya vimahali vinavyoambikwa kiambishi tamati cha mahali *-ni* na vile ambavyo ni majina mahususi ya mahali, imebainika kwamba, kwa kuzingatia tabia za kimofolojia, kisemantiki na kisintaksia vimahali vina tabia za vielezi. Kwa upande mwingine, vimahali hivyo huweza kuwa nomino pale vinapodhihirisha tabia za nomino. Hivyo, kwa kutumia nadharia ya Sampuli Kifani, hususani msingi wa mwingiliano wa kikategoria ni dhahiri kwamba vimahali ni maneno yenye mwingiliano wa kikategoria.

## Marejeleo

Amidu, A. A. (2007). Why locative marking in Kiswahili Bantu is not that simple. *The Linguistic Association of Korean Journal*, *15*(3), 21–42.

Baker, M. C. (2003). *Lexical categories: Verbs, nouns and adjectives*. United Kingdom: Cambridge University Press.

Bresnan, J., & Kanerva, J. M. (1989). Locative inversion in Chichewa: A case study of factorization in grammar. *Linguistic Inquiry*, *20*, 1–50.

Buberwa, A. (2016). *Mofolojia ya majina ya mahali ya Kiswahili na Kihaya katika jamii ya Wahaya: Uzingativu wa masuala ya kiisimujamii*. Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Dar es Salaam: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Geeraerts, D. (1984). Prototype theory and diachronic semantics: A case study of Indogemansche. *Forschungen, 89*,1–32.

Gleason, H. A. (1965). *Linguistics and English grammar*. New York: Holt, Rinehart and Winston.

Hyman, L. M., & Duranti, A. (1982). On the object relation in Bantu. *Syntax and Semantics*, 15, 217–239.

Kahigi, K. K. (2005). The Sisumbwa noun: Its classes and derivation. *Occasional Papers in Linguistics, 1*, 117–154.

Katamba, F., Dobrovolsky, M., & O'Grady, W. (1996). *Contemporary linguistics: An introduction*. United Kingdom: Pearson Education Limited.

Keenan, E. L. (1976). Towards a universal definition of subject, katika C. N. Li. (mh.), *Subject and Topic* (uk. 303 – 333). New York: Academic Press.

Kroeger, P. R. (2004). *Analysing syntax: A lexical functional approach*. Cambridge: Cambridge University Press.

Lambert, H. E. (1957). *Studies in Swahili dialect*. East African Swahili Committee.

Mdee, J. S. (1999). *Sarufi ya Kiswahili: Sekondari na vyuo*. Dar es Salaam: DUP.

Mkude, D. J. (2005). *The passive constructions in Swahili*. Tokyo: Research Institute for Languages and Cultures of Asia and Africa (ILCAA).

Ngunga, A., Mpofo-Hamadiziripi, N. (2013). A study of Bantu locatives: The case of Shona and Yao. *Journal of LASU*, *1*, 44–55.

Polomé, E. C. (1967). *Swahili language handbook*. Washington, DC: Center for Applied Linguistics.

Rosch, E. (1977). Human Categorization, katika N. Warren (mh.), *Studies in Cross-cultural Psychology, 1* (kur.1–49). London: Academic Press.

Rugemalira, J. M. (2004). Locative arguments in Bantu, katika A. Aknilabi & O. Adesola (Wah.). *Proceedings of the 4th World Congress of African Linguistics* (uk. 285–295). Köln: Rüdger Köppe Verlag.

Salzmann, M. D. (2004). *Theoretical approaches to locative inversion*. Unpublished Master's thesis. University of Zurich.

Taylor, J. R. (2003). *Linguistic categorization*. United States: Oxford University Press Inc.

Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili [TUKI], (1990). *Kamusi sanifu ya isimu na lugha*. Dar es Salaam: Educational Publishers and Distributors.

Van, V. R. (2001). Grammatical relations in ergative languages. *Studies in Languages*, 5, 361–394.